

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

(Barua zote zipelekwe kwa Mkurugenzi wa Jiji)

MKOA WA DODOMA

Tel.: 2324817/2321550
Fax: 2324817/2354817



Ofisi ya Mkurugenzi wa Jiji,
S.L.P.1249,
Dodoma.

Barua-pepe: cd@dodomacc.go.tz

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. HMD/E.20/6/49

Tarehe: 22 Oktoba, 2019

Kwa wananchi wote

**TANGAZO KWA UMMA KUHUSU UKOMO WA KUWA
MADARAKANI KWA WENYEVITI WA MITAA NA WAJUMBE
WA MITAA**

Kama ilivyotangazwa katika Tangazo la Serikali Na. 372 kwa mujibu wa Kanuni za Uchaguzi wa Mwenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Kamati ya Mtaa katika Mamlaka za Miji mwaka 2019; Kanuni ya 22 kuhusu ukomo wa kuwa madarakani (Mwenyekiti wa Mtaa na wajumbe wa Kamati ya Mtaa watakoma kushika nafasi hizo siku saba (7) kabla ya siku ya kuchukua fomu za kugombea uongozi chini ya Kanuni hizi).

Ninawataarifu kuwa, kuanzia tarehe 22 Oktoba, 2019 ndio ukomo wa kuwa madarakani kwa Wenyeviti na Wajumbe wa Mtaa ndani ya Jiji la Dodoma. Hivyo basi, wananchi wote mnajulishwa kuwa hakutakuwa na nyaraka yoyote au huduma yoyote itakayotambuliwa kisheria ikiwa imetolewa na Mwenyekiti wa Mtaa na Wajumbe wa Mtaa kuanzia tarehe 22 Oktoba, 2019, huduma

zote zitaendelea kutolewa na Watendaji wa Mitaa/Kata husika hadi pale Uchaguzi wa Viongozi utakapokamilika tarehe 24 Novemba, 2019.

Viongozi Bora wa Serikali za Mitaa ni chachu ya Maendeleo ni Haki na wajibu wako kujiandikisha, kugombea na kuchagua Viongozi Bora.


Dickson Nicholaus Kimaro
MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
JJI LA DODOMA

